## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI JUNI, 2021 NA MWELEKEO KWA MWEZI JULAI, 2021.

**Dondoo za tathmini ya Juni, 2021 na mwelekeo wa Julai, 2021:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Juni, 2021 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto la chini kwa mwezi Julai, 2021 nchini.

a) Katika kipindi cha mwezi Juni, maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye hali ya baridi. Hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi kadhaa vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani.

b) Katika mwezi Julai, 2021 hali ya baridi inatarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Vipindi vya upepo mkali pia vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, kanda ya ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2021.

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2021 maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye hali ya baridi. Hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki. Vituo vya hali ya hewa vya Igeri (kilichopo mkoa wa Njombe) na Uyole (Kilichopo mkoani Mbeya) vilipima viwango vya joto la chini kati ya nyuzi joto 5 na 9. Hata hivyo, vipindi kadhaa vya upepo mkali unaofikia kilometa 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo hususan ukanda wa pwani. Aidha, vipindi vichache vya mvua nyepesi vilijitokeza katika

maeneo machache ya ukanda wa pwani, ziwa Victoria pamoja na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JULAI, 2021

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la wastani inatarajiwa katika eneo kubwa la bahari ya Hindi. Hata hivyo, eneo la mashariki ya Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani wakati magharibi mwa Bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza kiasi cha upepo wenye unyevunyevu katika maeneo ya ukanda wa pwani. Hali ya joto la juu kidogo ya wastani inatarajiwa eneo la karibu na pwani ya Somali. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kuelekea baharini na hivyo kupunguza upepo wenye unyevu katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Kwa upande mwingine, hali ya joto la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kupunguza upepo wenye unyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Aidha, joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani katika maeneo ya kusini mwa Afrika inatarajiwa kusababisha hewa ya ubaridi kutoka maeneo hayo ya kusini.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2021

Hali ya joto la chini la kawaida kama ilivyozoeleka katika kipindi cha Kipupwe inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi ya nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi. Aidha, hali ya baridi zaidi inatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, kanda ya ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 hadi 23 katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko katika mikoa ya Tanga na Morogoro yanatarajiwa kuwa na viwango chini ya nyuzi joto 18. Hali ya ukavu itakayoambatana na vipindi vichache vya mvua nyepesi inatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 11 hadi 17 katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 11. Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua nyepesi inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 hadi 18 katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 14. Hali ya ukavu na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache kwa kipindi cha mwezi Julai.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 15 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu na vipindi vya upepo inatarajiwa kujitokeza.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 6 hadi 16 katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko pamoja na mkoa wa Njombe yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 6. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 19 hadi 22 katika maeneo mengi. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea pamoja na vipindi vichache vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 14 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 katika kipindi cha mwezi Juni, 2021. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**
***727B –00/2019***

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI AGOSTI, 2021

Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2021 hali ya ukavu na baridi itakayoambatana na vipindi vya upepo mkali. inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

## 2.4 USHAURI

Hali ya ukavu na upepo inaweza kuongeza upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo na kuathiri upatikanaji wa maji kwa mazao, mifugo na matumizi mengine. Hivyo, Jamii inashauriwa kuchukua hatua za tahadhari ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi mazuri ya maji na kujikinga ili kupunguza athari mbaya zinazoweza kusababishwa na hali ya hewa inayotarajiwa.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Julai, 2021 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**